

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



2 JUNI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA MBILI – TAREHE 2 JUNI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NISHATI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

351. MHESHIMIWA MOHAMED SULEIMAN OMAR (MALINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

- (a) Je, ni hatua gani zilizofikiwa kwenye mapambano dhidi ya Madawa ya Kulevya nchini;
- (b) Je, ni watu wangapi wamekamatwa kuanzia Mwaka 2019 – 2020 na wangapi wamehukumiwa.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

352. MHESHIMIWA FRANCIS ISACK MTINGA (IRAMBA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaainisha Mpaka kati ya Wilaya ya Mkalama na Hanang' eneo la Singa na Limbadau ili kuondoa taharuki kwa Wananchi.

WIZARA YA KILIMO:

353. **MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA (LULINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Serikali itawalipa Wananchi wanaodai miche ya mikoroshu deni ambalo ni la muda mrefu tangu Mwaka 2017.

354. **MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):**

● Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-●

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea miundombinu ya kisasa Akina Mama wa Tabora itakayoweza kukausha mboga kama Uyoga, Mchicha na Majani ya Maboga kwa njia ya kisasa zaidi ili kuwaongezea kipato;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha masoko ya ndani na nje ya nchi ili Akina Mama wa Tabora wanaokausha mboga waweze kuuza kwa faida.

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA
YA HABARI:**

**355. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS SAID
GULAMALI (MANONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa
Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka
mawasiliano katika Kijiji cha Matinje
Ikombandulu ambalo ni eneo la machimbo
na lina idadi kubwa ya watu ili kurahisisha
biashara katika eneo hilo.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

**356. MHESHIMIWA ROSE CYPRIAN TWEVE
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na
Sheria:- Kumekuwepo na mkangayiko wa
tafsiri ya umri wa miaka 18 katika Sheria
mbalimbali ikiwemo Sheria ya Mtoto na
Sheria ya Kanuni za Adhabu na kupelekea
kuvunja misingi ya Katiba:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuzifanyia
mapitio Sheria hizo hususan Kifungu cha
131 (2) cha Sheria ya Kanuni za Adhabu.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

357. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti mfumuko mkubwa wa bei za bidhaa ulioanza tangu Desemba, 2020 ambao umefanya gharama za maisha kupanda.

WIZARA YA MAJI:

358. MHESHIMIWA SILVESTRY FRANCIS KOKA (KIBAHA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Jimbo la Kibaha Mjini bado lina changamoto kubwa ya maji katika maeneo ya Kata za Mbwawa na Pangani; na Mradi wa Ujenzi wa matanki ya maji unakwenda kwa kusuasua.

Je, ni lini Mradi huo utakamilika ili Wananchi wa Kibaha Mjini waondokane na adha ya maji.

**359. MHESHIMIWA ABEID IGHONDO
RAMADHANI (SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:

Je, ni lini Serikali itavipatia huduma ya maji safi na salama Vijiji vya Kinyamwenda, Igauri, Matumbo, Itamka na Msimihi katika Jimbo la Singida Kaskazini.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**360. MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO
MGUNGUSI (MALINYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Sehemu kubwa ya maeneo ya Kilimo cha Mpunga Malinyi imemegwa na Mamlaka ya Wanyamapori (TAWA) kwa mipaka mipya iliyowekwa Mwaka 2017 bila maridhiano na Wananchi wa sehemu ya bonde la Kilombero:-

Je, Serikali haioni kuwa ni vema kufanya upya mapitio shirikishi kwenye mipaka ya eneo la Hifadhi.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NISHATI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**DODOMA
02 JUNI, 2021**

**N. J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**

